OFISI YA RAIS
IKULU

# MPANGO WA KURASIMISHA RASILIMALI NA BIASHARA ZA WANYONGE TANZANIA

MKURABITA

# MAELEZO KWA WAMILIKI MALI NA WAFANYABIASHARA WADOGO WADOGO NA KATI

Yametolewa na :

Program Management Unit.
DAR ES SALAAM 15 / 02/ 2006

**OFISI YA RAIS**
**IKULU**

# MPANGO WA KURASIMISHA RASILIMALI NA BIASHARA ZA WANYONGE – TANZANIA (MKURABITA).

## MAELEZO KWA WAMILIKI MALI NA WAFANYABIASHARA WADOGO WADOGO NA KATI

### 1. UTANGULIZI.

Tarehe 30 Septemba, 2003 Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliwaeleza Wananchi juu ya nia ya Serikali ya kuanzisha mpango utakaosaidia kurasimisha rasilimali na biashara za wanyonge walio katika sekta isiyo rasmi.

Na katika hotuba yake ya kila mwezi ya tarehe 30 Novemba, 2004 Mheshimiwa, Rais alitangazia Taifa kuwa Mpango umeanza rasmi tokea katikati ya mwezi Oktoba 2004.

Mpango huu ni sehemu ya mkakati wa kuendeleza uchumi na kuondoa umaskini.

Uchumi wa kisasa ambao unaendelea kuboreka hapa nchini umejengeka na unaendeshwa kwa mujibu wa sheria na kanuni rasmi za kiutawala.

Ni dhahiri hata hivyo kuwa Watanzania wengi hasa wale wa kipato cha chini vijijini na mijini wanamiliki mali, kufanya biashara na shughuli nyingine za kiuchumi kwa kutumia taratibu ama kanuni zinazotokana na mila na desturi za jamii husika na zisizotambulika katika mfumo wa sheria zilizopo.

Kanuni na taratibu ambazo hazitambuliki katika mfumo rasmi wa kumiliki mali na kufanya biashara ni kikwazo katika kuwashirikisha wadau wake kwenye uchumi wa soko rasmi kitaifa na kimataifa.

## 2. DHANA YA MKURABITA.

Dhana ya Mpango huu ni ushirikishwaji wa Watanzania walio wengi katika mfumo wa kitaifa wa umilikaji mali na uendeshaji biashara kama njia mojawapo ya kupiga vita umaskini na hivyo kuboresha maisha.

## 3. MADHUMUNI.

Madhumuni ya MKURABITA ni kuandaa mfumo wa kitaifa wa umiliki mali na uendeshaji biashara utakaoanisha na kuboresha kanuni na taratibu zinazotumiwa na makundi mbali mbali nchini na kuwa na mfumo mmoja wa kisheria, ili walengwa waweze kuutumia mfumo huo kupata mitaji ya kugharamia shughuli zao kadri ya utashi wao. Na pia wawe washiriki katika uchumi wa soko la ndani na nje ya nchi.

## 4. WALENGWA.

Walengwa mahususi wa mpango huu ni Watanzania, wanawake, wanaume na vijana wanaomiliki mali na kuendesha biashara katika sekta isiyo rasmi.

## 5. UTARATIBU NA HATUA ZA URASIMISHAJI.

Serikali imeamua kutumia utaalamu wa Taasisi ya Uhuru na Demokrasia kutoka Lima-Peru (Institute for Liberty and Democracy) inayoongozwa na Bw. Hernando de Soto, ambaye ni bingwa wa sekta isiyo rasmi anayetambulika dunia kote.

Kwa kutumia taaluma hii mpango wa urasimishaji umegawanyika katika sehemu kuu nne, nazo ni:-

5.1 Tathimini ya sekta isiyo rasmi ambapo utafiti utafanywa kubaini :

- (i) Ukubwa wa Sekta isiyo rasmi (makadirio ya wadau halisi) thamani yake katika uchumi wa nchi, kanuni na taratibu za uendeshaji, na mahali shughuli zilipo.

(ii) Vikwazo vinavyowazuia wahusika kuingia katika sekta rasmi au vivutio vinavyowafanya wapendelee kuwa katika sekta isiyo rasmi.

(iii) Mapungufu au vikwazo vya kisheria katika kumiliki mali na kufanya biashara.

Hatua hii ambayo utekelezaji alianza katikati ya mwezi Octoba, 2004 imechukua miezi kumi hivi na umekamilika na repoti kuwasilishwa rasmi kwa Mheshimiwa Rais tarehe 5 Octoba, 2005.

Taarifa (Report) itakayotolewa itazingatia pia mapendekezo ya awali ya maboresho yatakayohitajika.

## 5.2 MAANDALIZI YA MABORESHO (REFORM DESIGN)

Kwa vile Lengo ni kuwa na mfumo mmoja wa Sheria za umilikaji mali na uendeshaji biashara, maboresho yatalenga katika:

- Kuainisha na kuboresha kanuni zinazotumika sasa katika sekta isiyo rasmi ili ziwe msingi wa mfumo mpya.
- Kupendekeza marekebisho ya sheria au utayarishaji wa sheria mpya za umiliki mali na uendeshaji biashara ili ziunganishwe na kanuni za kijamii zilizoboreshwa.
- Kupendekeza mfumo wa utekelezaji, kubaini taasisi husika na kugawa majukumu.
- Kuandaa mfumo wa ushirikishwaji wa wadau.
- Kutathimini gharama za utekelezaji wa mpango mzima wa urasimishaji na kuweka vigezo au viashiria (indicators) vya kutathimini mafanikio.

Katika hatua hii mpango huu utaainishwa kikamilifu na MKUKUTA na kudhihirishwa zaidi katika mipango ya ki-sekta kama vile marekebisho ya sheria za ardhi, biashara, viwango na hata maendeleo ya jamii.

## 5.3 UTEKELEZAJI WA MABORESHO.

Utekelezaji wa hatua mbalimbali za kurasimisha rasilimali na biashara za wanyonge utafuata mara tu wadau watakapouafiki mpango wa maboresho na serikali kupata fedha, na nyenzo nyingine za utekelezaji.

Katika hatua hii pia mfumo wa kupata taarifa za utekelezaji (feed back) ili kuboresha mikakati ya urasimishaji utaanzishwa ikiwa ni pamoja na kituo cha kitaifa cha kumbukumbu (National Data base and record keeping) kitakachowezesha kuwa na taarifa kamili za sekta isiyo rasmi na mwenendo wake katika jamii.

Inategemewa kuwa tekinologia za kisasa katika upimaji, ardhi, uchoraji ramani na utunzaji kumbukumbu kwa kutumia teknologia za mawasiliano vitatumika ipasavyo.

## 5.4 KUIMARIKA KWA MITAJI NA UTAWALA BORA.

Hatua ya nne na ya mwisho katika mchakato mzima ni kutengeneza na kutekeleza taratibu ya kuziunganisha rasilimali zilizo rasimishwa na masoko rasmi nchini na nje ya nchi ili wadau waweze kutumia rasilimaji zao kuongezea mitaji kutoka katika masoko rasmi ya mitaji na hivyo kuboresha vipato vyao na pato la taifa kwa ujumla. Kwa kuzifanya shughuli zao ndani ya mfumo rasimi utawala bora utaimarika pia pato la Taifa litaongezeka.

## 6. MAENDELEO NA MATARAJIO HADI SASA.

### MATOKEO YA TATHMINI YA SEKTA ISIYO RASMI

Utafiti wa takribani miezi kumi imethibitisha kuwa:-

- Sekta isiyo rasmi ina thamani kubwa kiuchumi ikiwa inahozi mitaji mfu yenye thamani ya dola za kimarekani bilioni 28.09 kwa Tanzania bara na 1.21 kwa Tanzania Zanzibar.

Mtaji mfu mijini unakaribia dola za Kimarekani bilioni 11.60 kwa Tanzania bara, Dar es Salaam ikiwa na dola bilioni 3.5 yaani asilimia 30.

Mtaji mfu huu ni pamoja na thamani ya ardhi kwa makazi, kilimo na shughuli nyingine za kiuchumi.

Tathmini hii pia imebaini mambo mengine makuu mawili yafuatayo:-

(i) Watanzania wengi kwenye sekta isiyo rasmi wameasisi kanuni na taratibu za kumiliki mali na kufanya biashara ambazo zinakubalika miongoni mwao japo zipo nje ya mfumo rasmi wa kisheria.

(ii) Sheria zilizopo za umiliki mali zina vikwazo vingi na gharama kubwa zinazowafanya Wanyonge waziepuke.

Kutokana na tathmini hii imekubaliwa kuwa kanuni na taratibu na taasisi zinazotumiwa sasa na Wanyonge katika kufanya biashara na kumiliki mali ziboreshwe ili hatimaye ziwe msingi wa kujenga mfumo mpya wa kitaifa wa umiliki mali na kufanya biashara.

Imekubaliwa pia sheria za sasa za umiliki mali zifanyiwe marekebisho ili nazo ziwe sehemu muafaka katika mfumo mpya uliotajwa juu.

**CHANGAMOTO NI KUJENGA MAWASILIANO YATAKAYOWEZESHA KUFIKIA MAKUBALIANO NA WADAU WOTE JUU YA LENGO HILI.**

Hatua ya Pili ya Mpango huu ni kufanya maboresho yatakayoridhiwa na wadau ili kufikia lengo hilo.

Sambamba na changamoto hiyo katika maboresho wadau wana hamu ya kuona baadhi ya matunda ya Mpango mapema zaidi hata kabla ya maboresho kukamilika takribani baada ya miaka miwili hivi.

Hivyo yatafanyika maboresho madogo madogo yanayolenga kuweka msingi wa mabadiliko makubwa yajayo baada ya miaka miwili iliyotajwa.

Haya ni pamoja na kuandaa mfumo wa kuwashirikisha walengwa katika kuzibaini kero zao kuzipa kipaumbele na kuandaa mipango ya kuziondoa kwa kutumia uwezo wao na fursa zilizopo nchini. Hatua zitachukuliwa kwa kutumia asasi zilizopo kutoa mafunzo kwa walengwa na kuwezesha kuanza hatua za kurasimisha biashara zao na rasilimali zao bila kuathiri maboresho yanayotarajiwa.

Kwa kifupi tutaanza katika siku za karibuni:-

- Kuwasilisha kwa Wadau na umma ripoti hii ya tathmini ili kuibua mjadala utakaochangia katika kuboresha kanuni na taratibu za kijamii zitakazooanisha na sheria zitakazorekebishwa kuunda sheria na kanuni mpya.

- Kuhakiki matokeo haya ya tathmini ili kuwa na takwimu za msingi (base line) itakayotumika kupanga na kuratibu urasimishaji.

- Kuweka utaratibu wa kujenga uwezo wa walengwa katika kutumia rasilimali zao kupata mtaji.

- Kuwezesha walengwa kuanzisha vikundi, vyama rasmi (association's za kisekta) zitakazoweza kuwakilisha katika kujiletea maendeleo.